**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI MANDAWA,**

**S.L.P 02**

**RUANGWA**

**14/12/2020**

**KUMB. Na MASS/S.1898/F1/021**

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI….**……………………………………..**

**YAH: <u>MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021 KATIKA SHULE YA SEKONDARI MANDAWA</u>.**

Nachukua nafasi hii kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii, nakupongeza sana kwa mwanao kufanya vizuri katika mtihani wa darasa la saba.

Shule ya sekondari Mandawa ipo umbali wa km 39 kaskazini mwa Halmashauri ya wilaya ya Ruangwa. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021.**

**MAHITAJI MUHIMU**

Mwanafunzi anapaswa kuja shuleni akiwa amekamilisha mahitaji yafuatayo:-

- Daftari 15, mkebe wa hisabati (mathematical set), kalamu (peni) na penseli za kutosha, begi la kubebea daftari na Dictionary.
- File 2
- Mchango wa bima ya afya Tsh. 5,000/=
- Bando la karatasi (Rim paper) **2** kwa mwaka. ( muhula wa kwanza RIM 1 na muhula wa pili RIM 1).

**<u>SARE ZA SHULE</u>**

A. **<u>WAVULANA</u>**
   - Suruali mbili (2) za kijani, ambazo zinapatikana shuleni.
   - Shati mbili (2) nyeupe za mikono mifupi tetroni
   - Viatu vyeusi vyenye soli fupi, vya kupiga rangi na vya kufunga na Kamba, (kidamu)
   - Soksi nyeupe
   - Tai
   - T-shirt ya blue yenye nembo ya shule inapatikana shuleni kwa Tsh. 10,000/=
   - Sare za michezo (bukta na T-shirt rangi ya bluu na raba au viatu vya michezo)

B. **WASICHANA**

Sketi mbili (2) za kijani zinazovuka magoti.

- ❖ Shati mbili (2) nyeupe za mikono mifupi tetroni
- ❖ Viatu vyeusi vyenye soli fupi vys kupiga rangi (Bajaji haziruhusiwi kabisa)
- ❖ Soksi ndefu nyeupe
- ❖ Tai
- ❖ T-shirt ya blue yenye nembo ya shule inapatikana shuleni kwa Tsh. 10,000/=
- ❖ Hijabu (rangi ifanane na sare za shule)
- ❖ Sare za michezo (bukta na T-shirt rangi ya bluu na raba au viatu vya michezo)
- ❖ Sketi mbili za kijani, ambazo zinapatikana shuleni.

**VIFAA VYA USAFI**

- ❖ Ndoo ndogo la lita 10
- ❖ Fagio la chelewa
- ❖ Jembe lenye mpini, fyekeo/ panga (jembe lenye mpini lazima aje nalo, lakini fyekeo na panga alete kimojawapo)

**CHAKULA CHA MCHANA**

Shule inao utaratibu wa kutoa chakula cha mchana kupitia michango ya wazazi inayopaswa kuletwa na mwanafunzi wenyewe kama ifuatavyo:-

- ❖ Mahindi kilo 5, mbaazi kilo 3, chumvi ya unga paketi 1, pesa ya kusagia Tsh. 500.
- ❖ Fedha kwa ajili ya mpishi Tsh. 5,000/= kwa mwezi
- ❖ Mchango wa kununua sufuria kubwa ya kupikia chakula cha mchana Tsh. 1,000/=

Pamoja na fomu hii naambatanisha na

i. Nakala ya sheria za shule

ii. Medical Examination form ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali. (**fomu hii utaikabidhi kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni**)

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MANDAWA**

**OUR MOTTO** (KAULI MBIU YETU)

"**EDUCATION FOR PROGRESSIVE DEVELOPMENT**"
(ELIMU KWA MAENDELEO ENDELEVU)

**…………………………….**

**HALIMA H. MROPE**
**MKUU WA SHULE**
**0746-527347/0628-927418**

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI MANDAWA**

**S.L.P 02 RUANGWA**

## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE YA SEKONDARI MANDAWA

i. Mwanafunzi anapaswa kuwahi na kufuata ratiba inayomuhusu wakati wote awapo shuleni, akimbie kufuata mlio wa kengele inayomuita.

ii. Mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vilivyo katika ratiba ya shule na ajibidiishe katika masomo yake na ni kosa la kuadhibiwa mwanafunzi kupata chini ya 50% katika mitihani.

iii. Ni marufuku kupiga kelele darasani au kuongea kwa sauti kubwa katika eneo la shule.

iv. Kazi ni kipimo cha utu mwanafunzi atafanya kazi alizopewa kwa bidii na maarifa hadi kukamilisha kadri alivyoelekezwa

v. Mwanafunzi anapaswa kutunza mali yake, ya Umma na ya wenzake.

vi. Mwanafunzi haruhusiwi kuonekana sehemu za starehe kama baa, nyumba za kulala wageni (Guest house), na kumbi za disco.

vii. Heshima ni jambo la muhimu katika jamii mwanafunzi anatakiwa kusalimia watu wote waliomzidi umri kadiri ya stahihili zao, aonyeshe heshima kwa wanafunzi wenzake na jamii yote na kupokea mizigo ya waliomzidi.

viii. Siku za shule wanafunzi watatoka nje ya shule kwa kibali maalumu cha maandishi. Ruhusa itatolewa na mwalimu wa zamu. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare za shule anapotoka nje ya eneo la shule.

ix. Kwa vile masomo yote hufundishwa kwa **KIINGEREZA** isipokuwa **KISWAHILI**, mawasiliano yote ya kikazi yafanywe kwa lugha ya kiingereza. Ni kosa mwanafunzi kuzungumza lugha ya Kiswahili wakati wa kuwasalimia wanafunzi wenzake au walimu.

x. Lugha chafu (matusi) ni mwiko mwanafunzi anapaswa kuwa msafi kimwili, kimavazi na kiroho.

xi. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare iliyokubalika na shule kadiri ya ratiba iliyopo shuleni, avae sare ya shule anaposafiri safari za kishule, kumbuka kuchomekea shati/blauzi/T-shirt ndani ya suruali/sketi muda wote anapovaa sare ya shule na hairuhusiwi kuweka urembo wowote juu ya sare ya shule.,

xii. Mwanafunzi ajiepushe na makosa yafuatayo ambayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule mara moja.
   - Uasharati
   - Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya
   - Kupata mimba au kumpa mimba mwanafunzi mwenzake
   - Kupiga mtu yeyote (kupigana)
   - Wizi wa aina yoyote
   - Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
   - Kudharau bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa, fedha na viongozi halali wa vyama na serikali
   - Wizi wa mitihani au kudanganya wakati wa majaribio ya aina yoyote darasani.

…………………………

**HALIMA H. MROPE**
**MKUU WA SHULE**
**MANDAWA SEKONDARI**

**PRESIDENT'S OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**MANDAWA SECONDARY SCHOOL**
**P.O BOX 02**
**RUANGWA**
**14/12/2020**

**REF.NO.MASS/S.1898/F1/021**

TO THE MEDICAL OFFICER

**…………………………………….**

**REG: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF**

**……………………………………………………………**

Please examine the above-named pupil and give us a report regarding his/her suitability for undertaking secondary school studies.

**……………………………………**

**HALIMA HASSANI MROPE**

**MKUU WA SHULE**

**0628-927418**

1. Pupil's full name**……………………………………………………………………………….**
2. Blood**…………………………………………………………………………………………...**
3. Stool**…………………………………………………………………………………………**
4. T.B Test**……………………………………………………………………………………...**
5. Syphilis test**…………………………………………………………………………………….**
6. Urine examination**……………………………………………………………………………...**
7. Eye sight**……………………………………………………………………………………….**
8. Chest test**……………………………………………………………………………………….**
9. Hearing**………………………………………………………………………………………**
10. Spleen**………………………………………………………………………………………….**
11. Abdomen**……………………………………………………………………………………**
12. Pregnancy test (for girls)**……………………………………………………………………**

I certify that the above pupil is Fit/Unfit for secondary school studies. If unfit, please give reasons

**…………………………………………………………………………………………………**

**…………………………………………………………………………………………………**

**………………………………………………………………………………………………….**

Name of medical officer**……………………………………………………………………….**

Signature of medical officer**…………………………………………………………………**

Date**……………………………………………** Officer's stamp**……………………………….**